# ONDOKA KWANGU SHETANI

By: C . Mzena




2. Umeninyanyasa sana, maisha kuniharibia
Hasara ninaiona, ninateseka na dunia, Ondoka kwangu shetani sikutaki.
Moyo umeshauchana, hasara umenitia,
Na usalama hakuna, hivi nina angamia, Ondoka kwangu shetani sikutaki.

3. Umenipeleka pute, Nisilijue la kufanya,
Na faida nisipate, Nabakia kuwayawaya, Odoka kwangu shetani sikutaki.
Ninatubu dhambi zote, Na kuyaacha mabaya
Mwokozi nimfuate, Aniponye na hizaya, Ondoka kwangu shetani sikutaki.

4. Nafasi kwangu hauna, Nimekwishakushitukia
Kwa yakini nina nena, Ya nyuma sitayarudia, Ondoka kwangu shetani sikutaki
Hivi nasema hapana, Siyataki ya dunia
Nitamfata Rabana, Wala sibadili nia, Ondoka kwangu shetani sikutaki.